

**SHULE YA UPILI YA GATITU S.L.P. 327 ,01030 GATUNDU  
KISWAHILI KWA KIDATO CHA TATU, MUHULA WA PILI (2015)**

JINA..... *muda:saa mbili na nusu* .....  
DARASA:..... NAMBAARI:.....

Jibu maswali yote:

**A.MATUMIZI YA LUGHA**

1. Yakinisha:

Askari wasipopiga doria wala kushirikiana na raia hawatakuwa wametuhakikishia usalama. (Alama 2)

2.Nyambua vitenzi vifuatavyo katika kauli zilizo kwenye mabano. (Alama 3)

- i) Suka: (tendata).....  
ii) Ziba: (tenduka).....

3.Tambulisha vishazi katika sentensi zifuatazo:

a) Sisi tumeamua kuwasaidia iwapo tutashirikiana vilivyo. (Alama2)

b) Yule mwanafunzi stadi aliyaabika sana amefuzu vizuri.

4.Eleza mofimu katika maneno haya:

Walipoghairia:..... (Alama 3)

Kilichosahaulika:.....

5.Andika sentensi zifuatazo katika kauli zilizo mabanoni:

a)Yule mtotohawezikulishwachakula. (tendesheka) (Alama 3)

b) Wasichanawamekunywamaziwayote. (tendesheana)

c) Yule ndege alimnyea Ali utosini. (tendwa)

6. Andika kinyume.

(Alama 3)

Wazee weusi tititi waliingia ukumbini baada ya kupongezwa.

7. Tambulisha vielezi vyatnamna katika sentensi zifuatazo:

(Alama 2)

i. Babu yake alimkeea kijeshi kabla ya kumchapa kwa bakora.

ii. Mgonjwa alibebwa hobela hobela ndiposa alilia sana.

8. Bainisha virai katika sentensi zifuatazo:

(Alama 3)

Mgonjwa atapona baada ya wiki mbili hivi.

Nilimkuta katika hali ya majonzi.

Wowote watifu sana huwatuliza wazazi wao.

9. Onyesha kundi nomino na kundi tenzi

(Alama 1)

Kitoto chake cheusi kilikuwa hapa

**10. Geuza sentensi hii hadi usemi halisi:**

**Mwelekezi wake alimwambia kuwa angeweza kuwa mwindaji mashuhuri ikiwa angeyafuata mashauri vake.**

(Alama 3)

**11. Eleza matumizi ya ‘ki’ iliyopigwa mstari katika sentensi hizi.  
Ukirusha kipira hiki kitapotea.**

(Alama 3)

**Kitabu *ki* ndani ya kabati.**

12. Tunga sentensi yenyé muundo ufuatao:  $KN(N+V+E) + KT(T + I + F)$

(alama 2)

**b) Isimu-jamii**

**Asifiwe.....Nafurahia kuwa amekushindania Neno lacema katika**

- a) Mazungumzo haya hutokea katika muktadha gani? (Alama 2)  
.....

b) Fafanua sifa za lugha ya aina hii. (Alama 8)

B. FASIH

*i) Soma shairi lifyatalo kisha ujibu maswalli*

#### **1. Twamshukuru Mwenyezi, Kwawe wingi ukarimu**

Alo na kiti cha enzi. Mola wetu akramu...

**Kutupa kitu azizi, lugha kutakalamu.**

Lugha ni kitukitamu, uiuwapo kutumia

**2.Lugha mkuu mlezi , aleaye binadamu**

**Hata wanyama jambuzi, wema lugha wafahamu**

**Hafugu wasimulizi, izaayo tabasamu**

**Lugha huwa ni imamu, ujuwapo kutumia**

◦

**3.Lugha hodari mkwezi, akweaye tata ngumu,**

**Huzifyeka pingamizi, zizushazo uhasama,**

**Ikazidisha mapenzi, wapendanao kudumu,**

**Lugha huyeyusha sumu, ujuwapo kutumia,**

**4.Lugha ndiye mpagazi, mazito kuyahudumu,**

**Pia hupanga vizazi, pasi mbari kudhulumu,**

**Aidha hufanyakazi, ikawa mustakumu,**

**Lugha kwayo ni timamu, ujuwapo kutumia,**

**5.Lugha ni mpelelezi, maovu kuwa kasimu,**

**Huwatowa palo wazi, kashuhudia kaumu,**

**Yasifiwa na wajuzi, kuwa ni kituadhimu,**

**Lugha mkuu hakimu, ujuwapo Kutumia,**

**6.Lugha huizuwa kazi, kutatiza mahakimu,**

**Huwaacha kinywa wazi, wakili kitakalamu,**

**Muhalifu na jambazi, wakaishinda hukumu,**

**Urongo huwa timamu, ujuwapo kutumia,**

**7.Lugha iwe ni kiongozi, Kizungu au Kiamu,**

**Iwekapo waziwazi, silabi na tarakimu,**

**Huyakimu maongezi,yakasikizwa kwa hamu,**

**Lugha huwa ni muhimu, ujuwapo kutumia.**

**8.Lugha ni mapinduzi, wanyonge na wajukumu,**

**Kadhalika ni jahazi, ya nahodha muhitimu,**

**Kufa maji haiwezi, si vina si miizamu,**

**Lugha maji zam-zamu, ujuwapo kutumia,**

**Maswali.**

a)Pendekeza kichwa mwafaka kwa shairi hili

(Alama 1)

b) Eleza maudhui ya shairi hili

(Alama 3)

c)Eleza muundo wa shairi hili

(Alama5)

d) Andika ubeti wanne katika lugha ya nathari/ kawainda

(Alama. 3)

e) Taja huku ukitoa mifano, mbinu tatu za lugha alizotumia mshairi kuwasilisha ujumbe.  
(Alama3)

f) Kwa kutolea mifano onyesha idhini (uhuru) wa kishairi  
(Alama 2)

g) Eleza maana ya msamiati kama ulivytumika.  
(Alama 3)

i. Azizi:.....

ii. Uhasimu:.....

iii. Adimu:.....

## ii) FASIHI SIMULIZI

1. Eleza maana ya maigizo:  
(Alama 2)

1.ii) Fafanua sifa zozote nne maigizo.  
(Alama 8)

III) MSTAHIKI MEYA

Tamthilia ya Mstahiki Meya inaanishi hali halisi ya maisha katika miji ya bara la Afrika. Dhibitisha kauli hii kwa kuilejelea tamthilia hii.

(Alama 20)

AU

Mimi na Meya ni mfano wa maji na mafuta.

- a) Fafanua muktadha wa maneno haya (Alama 4)
- b) Taja na utoe mifano miwili yambinu za lugha zilizotumika katika dondo hili. (Alama 4)
- c) Fafanua sababu za kutofautiana kati ya warejelewa. (Alama 8)
- d) Eleza umuhimu wa msemaj . ( Alama 4)